

AZIMIO LA BUNGE NA. LA MWAKA 2022

**AZIMIO LA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA LA KURIDHIA
ITIFAKI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI YA KUIONGEZEZA MAMLAKA
MAHAKAMA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (PROTOCOL TO
OPERATIONALISE THE EXTENDED JURISDICTION OF THE EAST AFRICAN
COURT OF JUSTICE)**

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community) kwa mujibu wa mkataba ulioanzisha Jumuiya hiyo ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama tarehe 30 Novemba, 1999 na kuanza kutumika rasmi Julai, 2001;

NA KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia Itifaki za uanzishwaji wa Umoja wa Forodha (2004), Soko la Pamoja (2010) na Umoja wa Sarafu (2013), na inatekeleza itifaki hizo katika masuala ya biashara na uwekezaji nchini ambapo migogoro inaweza kutokea baina ya wanufaika wa Itifaki hizo na hivyo kuhitaji utatuzi wa tafsiri sahihi ya masharti ya Itifaki hizo kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa 1999 na matakwa ya Itifaki hizo tajwa;

NA KWA KUWA, Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa 1999 umeanzisha Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama chombo cha kusimamia haki na utii wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na kwa mujibu wa Ibara ya 27(2), Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki watakapoona inafaa, wanaweza kwa Itifaki ya Kuiongezea Mamlaka Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa masuala mengine mbalimbali;

NA KWA KUWA, Nchi wanachama kwa ridhaa ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wake wa 15 uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2013 kwa kuona umuhimu wa utekelezaji wa Itifaki za uanzishwaji wa Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja wa Sarafu zimeamua kuridhia Itifaki ya Kuiongezea Mamlaka Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoidhinishwa

na Mkutano wa kawaida wa 16 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 20 Februari, 2015;

NA KWA KUWA, ili Itifaki hiyo ianze kutumika ni lazima iridhiwe na Nchi Wanachama zote;

NA KWA KUWA, malengo ya Itifaki hiyo ni kuiongezea mamlaka Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kushughulikia masuala ya biashara, uwekezaji na sarafu ya pamoja;

NA KWA KUWA, Itifaki hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 3 (2) ikisomwa na Ibara ya 15 ya Itifaki ya Soko la Pamoja haiipi mamlaka Mahakama ya Jumuiya Afrika Mashariki kushughulikia masuala ya ardhi ambayo yameachwa kwa nchi wanachama;

NA KWA KUWA, Itifaki hiyo iwapo itaridhiwa na kuanza kutumika itawezesha utatuzi wa migogoro katika ngazi ya Kikanda itokanayo na utekelezaji wa Itifaki za Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja wa Sarafu na hivyo kuongeza utangamano katika Jumuiya na kukuza biashara na uwekezaji baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Dunia kwa ujumla;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na faida za Itifaki hiyo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge, katika Mkutano wake wa Nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kuiongezea Mamlaka Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, yaani ***The Protocol to Operationalise the Extended Jurisdiction of The East African Court of Justice.***
